

JILIPE MWENYEWE KWANZA

Sababu 50 Kwa Nini Unapaswa Kujilipa Kwanza Kabla Ya Kuwalipa Wengine Ili Kufikia Uhuru Wa Kifedha Na Utajiri.

ENG. TINDWA MARTIN (*Man Tindwa*)

Dibaji imeandikwa na Kocha Dr. Makirita Amani

YALIYOMO

SHUKRANI:.....	7
DIBAJI	9
SURA YA KWANZA	11
MAANA YA KUJILIPA MWENYEWE KWANZA	11
SURA YA PILI	13
MSINGI MKUU WA KUJILIPA MWENYEWE KWANZA.....	13
2.1 Jilipe Kuanzia Asilimia Kumi Ya Kila Kipato Unachoingiza.	14
2.2 Tenga Fungu La Pili Kwa Zaka, Sadaka Na Watu Wengine	15
2.3. Tenga Fungu La Dharura.....	16
2.4. Kuwa Mwenye Kipaumbele Kwenye Maisha Na Kutokujilinganisha Na Watu Wengine.....	16
Maswali Ya Kujiuliza Kwenye Sura Hii:.....	17
SURA YA TATU	18
FAIDA KUU YA KUJILIPA MWENYEWE KWANZA.....	18
3.1 Tenga Fungu La Maendeleo Binafsi	18
3.2 Tenga Fungu Kwa Ajili Ya Likizo Na Safari Za Kujifunza Vitu Mbalimbali.....	19
3.3 Umuhimu Wa Kutoa Zaka Au Sadaka kwa kutumia dhana ya Kujilipa Mwenyewe	19
3.4 Dhana ya Siku Sitini Na Sita (66) Za Kubadili Tabia Katika Kufanikisha Kujilipa Mwenyewe	20
3.5 Changamoto Ya Siku 100 Inaweza Kukusaidia Kutekeleza Jambo Hilo	21
SURA YA NNE	23
HATUA TATU ZA KUFANIKISHA ZOEZI LA KUJILIPA MWENYEWE KWANZA.....	23
4.1 Anzia Hapo Ulipo	23
4.2 Usisubiri Kuanza Na Kikubwa	24
4.3 Fanya Kwa Msimamo Kwa Kujirudiarudia Na Tabia Itajengeka.....	24
SURA YA TANO	26
SABABU 50 KWA NINI UNAPASWA KUJIILIPA MWENYEWE KWANZA	26
1. Upendo Unaanzia Kwako Na Kusambaa Kwa Wengine	26

2. Nguvu Zetu Zinapungua Kadri Umri Unavyozidi Kwenda	27
3. Ni Njia Pekee Ya Kushika Pesa Kubwa Ya Kwako Mwenyewe	28
4. Kupata Kiwango Cha Pesa Kitakachoweza Kukupitisha Salama Kwenye Changamoto za Maisha.	29
5. Utaepuka Dhana Ya Kuamini Fedha Ya Mafao Ni Ya Kwako	30
6. Utapunguza Utegemezi Baada Ya Kustaafu	31
7. Utapata Njia Bora Ya Kuama Kutoka Ngazi Moja Ya Biashara Kwenda Ngazi Nyingine	32
8. Ukijitoa Utapokea	33
9. Kupata Pesa Kwa Ajili ya Kutembelea Vivutio Vya Kitalii.....	33
10. Utaepuka Mtego Wa Kuongezewa Matumizi Ukipata Pesa	34
11. Utapata Pesa Ya Kuwekeza Kwa Muda Mrefu	35
12. Utapata Mtaji Kwa Ajili Ya Kutimiza Malengo Makubwa Ya Kibiashara Na Maisha.	37
13. Utaweza Kupata Pesa Kwa Ajili Ya Kujifunza Zaidi	37
14. Kuwa Na Ushiriki (Udhibiti) Mkubwa Kwenye Maisha Yako.....	38
15. Utaweza Kuwa Na Pesa Ya Kuweza Kuwekeza Kwenye Fursa Bora Ambazo Zinajitokeza Kwa Dharura.	39
16. Itakusaidia Kuvunja Minyororo Ya Tabia Mbaya Kuhusu Fedha	39
17. Utaweza Kuifanya Pesa Ikufanyie Kazi.....	40
18. Itakusaidia Kutengeneza Msimamo Na Tabia Bora Binafsi.....	41
19. Utakuwa Sehemu Ya Watu Wachache Waliofanikiwa Kwenye Jamii	42
20. Utaepuka Mikopo Mibaya Ambayo Inakupelekea Kuwa Maskini (Kausha Damu).	43
21. Utaweza Kupata Faida ya Maajabu Ya Nguvu Ya Riba Mkusanyiko	44
22. Utapata Kinga Dhidi Ya Msongo Wa Mawazo	44
23. Kujenga Kizazi Imara Ambacho Kitaweza Kuwa Na Ufahamu Wa Mambo Ya Pesa Mapema	45
24. Utaona Thamani Ya Muda Wako Ulioutumia Kufanya Shughuli Za Kuongeza Kipato	46
25. Utakuwa Kiongozi Bora Kwa Vijana	47
26. Utakuwa Umejikubali Mwenyewe Kwanza	48
27. Tutapunguza Deni Kubwa La Kuilaumu Serikali Na Watu Wengine.	49

28. Kipato Chochote Unachokipata Utakuwa Umekiongeza Thamani Zaidi Hapo Baadaye Na Kuweza Kukabiliana Na Mfumuko Wa Bei.	50
29. Utaepuka Mtego Wa Tamaa Ya Mali Pale Unapopata Mamlaka.	50
30. Utaweza Kutimiza Shauku Na Ndoto Zako Kubwa Ulizonazo.....	51
31. Itakusaidia Muda Wote Kuwa Kama Umeishiwa Kwa Sababu Umeshachukua Hatua Mapema.	52
32. Utaepuka Kisa Cha Kuhesabu Mayai Kama Vifaranga Kabla Ya Kutotolewa.	53
33. Utapata Njia Nyepesi Ya Kukusanya Mtaji Kidogo Kidogo.....	54
34. Utaepuka Kujipa Sifa Na Hadhi Ambazo Hauna Au Bado Haujazifikia.	55
35. Utakuwa Umejenga Mtazamo Sahihi Kuhusu Utajiri na Uhuru kwa kifedha Kwa Vitendo.....	56
36. Utaepuka Ushawishi Wa Kucheza Kamari.....	57
37. Utakuwa Imara Pale Mabadiliko Ya Asili Yatakapotokea Ambayo Yapo Nje Ya Uwezo Wetu.....	58
38. Utaepukana Na Mtego Wa Ushawishi Kwa Kutaka Pesa Nyingi Kwa Haraka (Kutapeliwa).....	59
39. Utaepuka Kufanya Kazi Za Shuruti Ukiwa Na Umri Mkubwa Mpaka Unakufa.	60
40. Utaepuka Kuwa Bomba Kubwa La Kupitisha Maji	61
41. Utakuwa Umetengeneza Tabia ya Kuweka Akiba	62
43. Utakuwa Na Uhuru Wa Kifedha Kwenye Maisha Yako	65
44. Utavunja Mkosi wa kuanza moja kwa kila kizazi kwenye koo au familia yako	65
45. Utaepuka Msongo Wa Mawazo Pale Kutakapotokea Mabadiliko Ya Kiuongozi. .	66
46. Utakuwa Mshauri Bora Na Mwenye Kujiamini	67
47. Utakuwa Na Pesa Ya Kutosha Ya Kuweza Kufanya Uwekezaji Mwingine	68
48. Utavunja Dhana Potofu Ambayo ipo Kwenye Jamii Kwamba Utajiri Ni Dhambi ..	69
49. Hakuna Mtu Atakuja Kukutoa Hapo Ulipo	70
50. Utakuwa Umpanda Mbegu Ya Kufikia Uhuru wa kifedha na Utajiri.....	70
SURA YA SITA	73
NJIA BORA ZA KUWEKA FEDHA AMBAYO UTAJILIPA MWENYEWE	73
SURA YA SABA.....	76
JINSI YA KUDHIBITI MATUMIZI YAKO ILI UWEZE KUPATA PESA YA KUJILIPA MWENYEWE KWANZA	76

Maana Ya Matumizi.	77
Aina Za Matumizi.	78
Kundi La Kwanza: Matumizi Ya Muhimu Na Lazima.....	78
Kundi La Pili: Matumizi Muhimu Lakini Siyo Ya Msingi	78
Kundi La Tatu: Matumizi Ya Starehe	79
SURA YA NANE	81
SEHEMU AMBAZO UNaweza KUFANYA Uwekezaji BAADA YA KUPATA PESA AMBAZO UTAKUWA UNAJILIPA MWENYEWE KWANZA	81
Maana Ya Uwekezaji.	81
Aina Kuu Sita Za Uwekezaji.....	83
Aina Ya Kwanza: Uwekezaji Kwenye Soko La Hisa	84
Aina Ya Pili Ya Uwekezaji: Uwekezaji Kwenye Mali (Majengo)	85
Aina Ya Tatu Ya Uwekezaji: Uwekezaji Kwenye Hati Fungani (Bonds).....	86
Aina Ya Nne: Uwekezaji Kwenye Mfuko Wa Pamoja (Mutual Funds).....	87
Aina Ya Tano: Kuwa Na Akaunti Maalumu Ya Benki.....	90
Aina Ya Sita: Kufungua Akaunti Ya Fedha Za Kigeni	91
SURA YA TISA	92
NJIA BORA ZA KUKUSAIDIA KULINDA KILE UNACHOJILIPA MWENYEWE	92
Bima.....	92
Bima Ya Afya.	92
Bima Ya Maisha.....	93
Bima Ya Ulemavu.	93
Bima Ya Majengo (Nyumba).....	94
Bima Ya Gari.....	94
HITIMISHO.....	95
VITABU VYA REJEA.....	96
KUHUSU MWANDISHI	97

SHUKRANI:

Kuandika kitabu siyo kazi rahisi. Nimekuwa nikiandika tafakari za hamasa kila siku kwenye vikundi mbalimbali vya whatsapp. Tafakari hizo zimekuwa zikigusa maisha ya watu hasa kwa kuwatia moyo kwenye kuchukua hatua kwa kutoka pale walipo na kwenda mbele zaidi. Pamoja na kuandika huko tafakari za kila siku, bado kuandika kitabu ni kazi ngumu. Bila msaada wa watu wengine kitabu kama hiki kisingewezekana.

Ni vigumu sana kuwataja watu wote waliofanikisha kuandika kitabu hiki na kingine, lakini kila ambaye ninajuana naye na nimewahi kushirikiana naye kwenye kujifunza au mazungumzo ya kimaisha mchango wake umesaidia sana kwenye kusaidia kuandika kwa kitabu hiki.

Ninamshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema na baraka aliyetujaalia uzima mpaka kufikia uwezo wa kuandika kitabu hiki siku hii ya leo. Wengi walitamani kutimiza ndoto kama hii hawajaweza, hivyo ni kwa neema tu katika kufikisha malengo kama haya.

Ninaishukuru familia yangu Baba, Mama na wanafamilia wote kwa maombi yao ya kila siku bila kuchoka, kwa upekee na kwa umuhimu mke wangu Elizabeth pamoja na watoto Lawrence, Macarius na Martina ambao wamekuwa wakinikosa mara kwa mara hasa hata muda ule wa mapumziko ambapo walitamani nicheze nao walijikuta wakiwa peke yao. Uvumilivu wao mkubwa umekuwa msaada mkubwa katika kukamilisha kazi hii ambayo imenichukua karibu miezi kadhaa kuifanya kwa umakini mkubwa.

Ninamshukuru sana kocha wangu wa mafanikio Dr. Amani Makirita kwa usimamizi wake mkubwa ambao mara zote umekuwa unatutia moyo kukaa kwenye mchakato na kuchukua hatua siku hata siku hata kama hatua hizo ni kidogo. Maana hizi hatua ndogondogo ndizo zinapelekea kufanya vitu tofauti hasa kwa ile kanuni yake ya siku yako ya leo isifanane na kesho. Kupitia mafunzo yake na semina nimeimarika mpaka kuweza kuchukua hatua hii ya kuandika kitabu.

Pia nimshukuru Mwandishi mbobezi ndugu Godius Rweyongeza maarufu kama Mr. Songambe kwamba kwa vitabu vyake ambavyo vimekuwa mwongozo na msaada mkubwa pale nilipoanza kuchukua hatua ya kuandika kitabu hiki ambavyo vimekuwa mwongozo mkubwa sana katika kukamilisha kazi. Pia napenda kumshukuru sana Mwalimu Emilian Busara kupitia mafunzo yake ya mtandao wa youtube japo sijawahi kuonana naye lakini kupitia kazi zake nimekuwa nikipata nguvu zaidi ya kuchukua hatua kwenye masuala ya uwekezaji Mungu ambariki sana. Namshukuru Dr. Harris Kapiga wa Clouds FM na Wakili Msomi Henry Mwinuka kupitia kipindi chao cha Temino najifunza mengi zaidi yahasuyo maarifa wanayotoa na watu wanaowaalika. Kwa pekee nawashukuru Dr. Isaack Maro wa Clouds Media Group na wasaidizi wake Amani na Douglas kwani kupitia kipindi chao cha Njia Panda pia wamenipa nguvu kubwa sana ya

kuchukua hatua ya kuandika kitabu hiki hasa kwa yale ambayo watu wanayapitia na kuyaelezea katika kipindi chao na kuona kuna umuhimu wa kuelezea dhana hii ya kujilipa mwenyewe ili kupunguza sehemu ya njia panda hizo ambazo zinawakabili watu hasa zile ambazo zinaweza kudhibitiwa kwa mifuko ya dharura binafsi ambayo tunaweza kuiweka, nawapongeza wanafanya kazi kubwa ambayo jamii inaitambua na kuithamini.

Pia napenda kumshukuru Dr. John Kafuku kwa hamasa aliyoniongezea kwenye somo lake la ujasiriamali kwenye masomo ya shahada ya uzamili ameniongezea hamasa na nguvu zaidi ya kukamilisha kazi hasa kupitia masomo yake na ndoto zake zinazoendana na uhalisia wa somo analolifundisha kama mfano wa kuigwa.

Mwisho kabisa ninawashukuru wanachama wote wa KISIMA CHA MAARIFA hasa kupitia programu maalumu ya BILLIONAIRE IN TRAINING (BIT) ambapo ilikuwa sehemu na chachu kubwa ya mtu kuchukua hatua kwenye maisha bila kukoma na hivyo kuongeza hamasa katika kukamilika kwa kazi hii ya kuchapa kitabu hiki.

DIBAJI

DIBAJI – JILIFE MWENYEWWE KWANZA.

Mtu yeyote mzima, ambaye amefanya kazi yoyote ya kuingiza kipato, ukijumlisha fedha zote ambazo amewahi kupokea ni nyingi sana kuliko alizonazo. Yaani hata mtu ambaye yupo kwenye madeni makubwa, bado ukijumlisha fedha ambazo amewahi kulipwa ni nyingi.

Swali kubwa sana la kujiuliza ni nini kinapelekea watu ambao wanaingiza kipato kujikuta wamebaki hawana kitu kabisa? Mwandishi Grant Cardone amewahi kusema alipokuwa na miaka 25 alikuwa na fedha kidogo kuliko alivyokuwa na miaka 11. Akimaanisha akiwa na miaka 25 alikuwa na madeni mengi kuliko alivyokuwa na miaka 11.

Ukweli ni kwamba, licha ya watu kuingiza kipato, bado wamekuwa wanabaki hawana kitu kwa sababu ya kushindwa kujilipa wao wenyewe. Wanakuwa tayari kuwalipa watu wengine wote, lakini wanajisahau wao wenyewe. Mwishowe wanakuwa kama madalali wa fedha zao, wanazipokea na kuzipeleka kwa wengine.

Jambo la kufurahisha ni watu huwa hawakosi sababu kwenye jambo lolote wanalofanya au kushindwa kufanya. Ukimuuliza mtu yeyote anayeingiza kipato kwa nini anatomia chote mpaka kinaisha, anakujibu kipato chake hakitoshelezi. Hivyo akishatumia, habakiwi na chochote cha kujilipa yeye mwenyewe.

Kwa haraka unaweza kukubaliana na sababu hiyo, lakini ni mpaka pale utakaporudi kwenye uhalisia na kugundua kwamba, fedha haijawahi kukosa matumizi. Fedha ikiwepo, matumizi yatapatikana tu.

Kitabu hiki cha JILIFE MWENYEWWE KWANZA ni mwongozo sahihi wa kifedha kwa mtu yeyote anayetaka kujijengea uhuru wa kifedha na utajiri kwa kuanzia pale alipo sasa. Kama jina linavyojieleza, zoezi la kujilipa mwenyewe linapaswa kuwa la KWANZA. Yaani unapopokea kipato chako, kabla hujafanya matumizi yoyote, unianza kwa kutenga pembeni fungu la kujilipa, halafu kinachobaki ndiyo unatumia.

Ni kwa kutumia kanuni hiyo ya KUJILIPA MWENYEWWE KWANZA ndiyo unaweza kujilipa hata kama kipato chako ni kidogo kiasi gani. Unapoweka vipaumbele sahihi kwenye matumizi ya fedha zako, kwa kuanza na kujilipa, unaweza kutumia kipato kidogo ulichonacho kujenga utajiri mkubwa.

Neno utajiri limewatesa sana watu wengi. Watu wamehangaika na mambo mengi sana kupata utajiri. Wapo walioiba na kudhulumu wengine, na utajiri walioupata haukudumu. Wapo waliocheza bahati nasibu na kamari na wengi walikosa, huku wachache waliopata nao wakishindwa kudumu na utajiri. Na wapo waliotumia njia za kishirikina na bado wasipate utajiri unaodumu.

Mambo mengi kwenye maisha huwa ni rahisi, lakini watu huwa wanahangaika kuyafanya kuwa magumu. Ikiwepo swala la utajiri, mahangaiko yote ambayo watu wanayo juu ya utajiri, ni kujitesa tu. Kanuni ya kujenga utajiri ni rahisi na inayoeleweka na kila mtu. Na inasema hivi; **MARA ZOTE MATUMIZI YAWE MADOGO KULIKO KIPATO CHAKO.**

Kama utaamua kuachana na mambo mengine yote na ukaamua kukomaa na hilo moja tu, kwamba kwenye kila kipato unachoingiza matumizi yawe madogo kuliko kipato hicho na ukaenda hivyo kwa maisha yako yote, lazima utajenga utajiri. Huo ni uhakika, siyo kubahatisha. Utawezaje kuhakikisha mara zote matumizi yanakuwa madogo kuliko kipato? Jibu lipo ndani ya kitabu hiki, kwa kuhakikisha kwenye kila kipato unachoingiza, unajilipa wewe mwenyewe kwanza kabla hujaanza matumizi. Na kile unachojilipa hukiachi kiholela, bali unakiweka kwenye gereza ambapo huwezi kukifikia kirahisi. Yote hayo utajifunza kwa kina kwenye kitabu hiki.

Kwenye kitabu cha **MTAALA WA UTAJIRI** nilichoandika, nimeeleza kwa kina kwa nini utajiri au umasikini hauanzii kwenye kipato, bali kwenye fikra. Na ushahidi wa hili ni watu wawili wanaoweza kuwa wanafanya kazi au biashara ya aina moja, wanalingana kipato, lakini mmoja akajenga utajiri huku mwingine akibaki kwenye umasikini. Unaona na kufikiria nini ndiyo mahali utajiri au umasikini unapotengenezwa kwenye fikra zako. Kinachoonekana nje ni matokeo tu.

Kudihirisha hilo, angalia jinsi ambavyo watu wengi wanaopata fedha nyingi kwa mkupuo, labda wamepata mirathi, wamelipwa mafao au kushinda bahati nasibu, huwa wanaishia kuzipoteza haraka pia.

Eng. Tindwa Martin amefanya kazi kubwa ya kukujengea mtazamo sahihi wa kifedha kwenye kitabu hiki cha **JILIFE MWENYEW KWANZA**. Ni bahati ya kipekee kwako kupata kitabu hiki, hivyo kosome kwa kina, kielewe na kiweke kwenye matendo.

Matumaini yangu ni baada ya kusoma kitabu hiki, hutaichukulia tena fedha kwa namna ulivyokuwa unaichukulia awali. Kwa kila fedha inayopita kwenye mikono yako, iwe umelipwa kwa kazi, umepewa zawadi au hata umeokota, utaitendea kulingana na mafunzo unayoyapata hapa.

Nikutakie kila la kheri kwenye safari yako ya kujenga utajiri na uhuru wa kifedha ambayo unaianza kwa uhakika kwa mwongozo wa kitabu hiki. Familia yako, taifa lako na dunia kwa ujumla inahitaji matajiri wengi. Wewe unapaswa kuwa mmoja wa hao ili uweze kuwa na mchango mzuri kwa wengine.

Kocha Dr. Makirita Amani,

Daktari wa binadamu, Kocha wa mafanikio, Mwandishi na Mjasiriamali.

www.amkamtanzania.com

SURA YA KWANZA

MAANA YA KUJILIPA MWENYEWE

KWANZA

Kujilipa mwenyewe ni kitendo cha kujiweka wewe na familia yako wa kwanza kabla ya mahitaji mengine yoyote ya kifedha, kwa upande mwingine ni kuchukua sehemu ya kipato na kujiweka sehemu ambapo hautakitumia kwa muda maalumu. Sehemu hii ya kipato itatumika pale tu ambapo hutakuwa na nguvu za kufanya kazi moja kwa moja na pia kama sehemu ya kukuzwa mtaji kuongeza thamani ya kipato cha awali ulichopata. Sehemu hii unapaswa kuitoa kwenye kipato chako kabla hujafanya matumizi yoyote. Unapaswa kuanza kujilipa mwenyewe kwanza kabla hujaanza kuwalipa wengine kwa matumizi mbalimbali unayoyafanya. Jambo lingine muhimu na la msingi la kuzingatia kujilipa mwenyewe ni sehemu ya kujiheshimu, hivyo kama haujilipi mwenyewe kwa upande mwingine haujiheshimu wewe mwenyewe.

Kujilipa mwenyewe maana yake ni kujijali wewe mwenyewe kwani kama unavyofahamu kadri umri wako unavyozidi kusogea ndivyo nguvu zako zinapungua pia. Ukiwa kijana unaweza kufanya vitu vingi zaidi kuliko ukiwa mtu mzima. Kupitia nguvu ya kujilipa mwenyewe utaweza kupata kipato cha kuyaendesha maisha yako pale utakapokuwa umepoteza nguvu za kufanya kazi.

Kwa kawaida mtu ukipokea fedha huwa kuna matumizi ambayo unafanya. Unaweza kufanya matumizi kadha wa kadha kama kununua nguo, kulipa bili, kodi na vinginevyo. Ila cha kushangaza ni kwamba unakuwa umepokea fedha na imepita mikononi mwako, huku wewe ukiwa hujabaki na kitu chochote kile.

Hivyo dhana hii ya kujilipa mwenyewe ni ya kujijali nafsi yako kama kitu cha kwanza kabla haujafanya malipo mengine yoyote, ndio maana ukipanda ndege kabla haijaondoka unapewa tahadhari ya hatari ambazo zinaweza kujitokeza angani. Lakini unaelekezwa kwa undani zaidi kwa kuambiwa kuwa endapo itatokea hatari basi kuna kifaa cha hewa ambacho unaweza kutumia kujiokoa.

Kifaa hicho kinaweza kuwaokoa wengine pia. Lakini sasa unaambiwa unatakiwa uanze kujiweka wewe kwanza hicho kifaa, hata kama uko na mtoto wako unaambiwa anza kujiweka mwenyewe hicho kifaa. Hii ni moja ya dhana halisi inayoonesha maana ya kujilipa mwenyewe kwanza hata kwenye usalama wa kimaisha kama huu.

Mfano huo utuoneshe dhana halisi ya kuweza kuifanyia kazi na kuwa na msukumo wa kitu hiki cha kujilipa mwenyewe kwanza na kuweza kuchukua hatua kubwa kwenye maisha yako na kuweza kufikia malengo mkubwa ambayo umejiwekea.

Kwenye kipato chochote ambacho unaingiza unashauriwa kuweka pembeni kiwango cha chini angalau asilimia kumi kama sehemu ya kujilipa mwenyewe. Na siyo lazima uanze na asilimia kumi bali hiki ni kiwango cha chini ambacho kinashauriwa kuwekwa na kisipungue ili kuweza kuwa uhuru wa kifedha.

Lakini kwa nguvu ya hamasa ambavyo inabidi kwenda na vitendo anza hata kwa asilimia moja na utaweza kuongeza asilimia hiyo kadri muda unavyozidi kwenda na kufikia Asilimia kumi na zaidi ambayo inashauriwa na wataalamu ili kuweza kufikia uhuru wa kifedha na kujilipa mwenyewe kwani maarifa yanapaswa kwenda na vitendo.

KUPATA KITABU HIKI KIZIMA MPAKA MWISHO UTALIPIA
15,000/- KUPATA HARDCOPY
NA 10,000 KWA AJILI YA SOFTCOPY
Au wasiliana na 0758138087 au
BONYEZA HAPA KUPATA NAKALA YAKO
www.getvalu.co

KUPATA KITABU HIKI KIZIMA MPAKA MWISHO UTALIPIA
15,000/- KUPATA HARDCOPY
NA 10,000 KWA AJILI YA SOFTCOPY
Au wasiliana na 0758138087 au
BONYEZA HAPA KUPATA NAKALA YAKO
www.getvalu.co